

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Baruapepe : press@ikulu.go.tz  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

Des Moines - Iowa  
31 Oktoba, 2024

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa nchi za Afrika na wabia wake kufanya uwekezaji stahiki na kuimarisha ushirikiano ili kuleta mageuzi kwenye sekta ya kilimo barani Afrika na kuiwezesha kuchangia katika kuhakikisha usalama wa chakula duniani.

Rais Dkt. Samia amesema hayo wakati akishiriki Mjadala wa Kimataifa wa Chakula wa Norman E. Borlaug ulioandaliwa na Taasisi ya World Food Foundation mjini Des Moines, Iowa nchini Marekani. Jukwaa hilo lililoanzishwa kwa heshima ya mshindi wa Tuzo ya Nobel Dk. Norman E. Borlaug, anayejulikana kama "baba wa Mapinduzi ya Kijani", linalenga kukuza ushirikiano na uvumbuzi ili kushughulikia masuala ya usalama wa chakula duniani kote na kubainisha umuhimu wa kilimo katika kufikia maendeleo endelevu.

Majadiliano hayo yaliangazia changamoto kubwa za kilimo zinazokabili Afrika na kutafuta suluhu zinazoweza kutokana kupitia ushirikiano na wadau wa Marekani.

Katika mjadala huo, wadau wakubwa wa sekta ya kilimo nchini Marekani wametambua faida na kuonyesha nia ya kuanzisha ushirikiano na nchi za Afrika, na wamesisitiza manufaa ya teknolojia ya kilimo na utaalamu katika kuimarisha uzalishaji wa chakula barani Afrika.

Kwa upande wake Rais Dkt. Samia amesisitiza umuhimu wa kufanya kilimo cha kisasa zaidi ili kuimarisha usalama wa chakula. Aidha, amebainisha mchango muhimu wa Tanzania katika sekta ya kilimo barani Afrika, ambapo amesisitiza kuwa Tanzania bado ina fursa nyingi za uwekezaji kutokana na ardhi yenyе rutuba inayofaa kwa uwekezaji wa kilimo, uwepo wa nguvu kazi yenyе ujuzi stahiki na Serikali ambayo imejidhatiti kuchochea maendeelo ya kilimo.

Rais Dkt. Samia amesema uwekezaji ambao unafanywa na Serikali ya Tanzania katika sekta ya kilimo unalenga sio tu kukabiliana na uhaba wa chakula nchini Tanzania bali



pia kuchangia kutatua changamoto pana za usalama wa chakula zinazoikabili Afrika na dunia kwa ujumla.

Akizungumzia ukuzaji wa mnyororo wa thamani, Rais Dkt. Samia amesema anakaribisha uwekezaji unaolenga kuboresha mnyororo mzima wa thamani wa kilimo, kuanzia uzalishaji, usindikaji hadi upatikanaji wa masoko.

Majadiliano hayo pia yalitoa fursa kwa Viongozi wa Afrika na wadau wengine kujadili changamoto ambazo nchi zao zinakabili ana nazo kama vile uharibifu wa mazingira, uhaba wa maji, na athari za mabadiliko ya hali ya tabianchi.

Pembezoni mwa mikutano huo, Rais Dkt. Samia pia ameshiriki katika majadiliano na Viongozi wa Serikali ya Marekani, na wadau wa sekta binafsi waliopo katika sekta ya kilimo, kujadili fursa za uwekezaji na kuimarisha mnyororo wa thamani katika kilimo nchini Tanzania.

Kila mwaka mjadala huo wa kimataifa wa Norman E. Borlaug huleta pamoja wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo kwa lengo la kubadilishana maarifa na kutafuta suluhu za kutatua changamoto zinazotokana na njaa na lishe duniani na kuwaleta pamoja Viongozi kutoka katika bara zima la Afrika, pamoja na wawakilishi kutoka Serikali ya Marekani na sekta binafsi, hasa wale wanaojihusisha na kilimo.

Sharifa B. Nyanga  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

